



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

UTAFITI WA KILIMO WA MWAKA 2022/23

MATOKEO MUHIMU



SEPTEMBER, 2024



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2022/23

Matokeo Muhimu

Septemba, 2024



Kwa Msaada wa Kifedha wa



Kwa Msaada wa Kitaalamu Kutoka



**Food and Agriculture Organization
of the United Nations**

Orodha ya Majedwali	ii
Orodha ya Vielelezo	iii
Vifupisho vya Maneno	iv
Dibaji	v
Usuli	1
1.0 Utangulizi	1
1.1 Dhumuni la Utafiti	1
2.0 Matokeo Muhimu	2
2.1 Shughuli za Kilimo za Kaya	2
2.2 Umiliki wa Ardhi	2
3.0 Uzalishaji wa Mazao	5
3.1 Uzalishaji wa Nafaka	5
3.2 Uzalishaji wa Mazao Jamii ya Mizizi	5
3.4 Mazao Jamii ya Mikunde	7
3.5 Uzalishaji wa Mazao ya Biashara	8
3.6. Uzalishaji wa Migomba, Parachichi na Nyanya	9
3.6 Majanga kwenye Eneo Lililopandwa Mazao	10
3.7 Matumizi ya Mazao	11
3.7.1 Nafaka	11
3.7.2 Mazao Jamii ya Mizizi na Viazi	11
3.7.3 Mazao Jamii ya Kunde	12
3.7.4 Mbegu za Mafuta na Karanga	13
3.7.5 Mazao ya Biashara	13
3.7.6 Matunda na Mbogamboga	14
4.0 Umwagiliaji na Matumizi ya Pembejeo	16
4.1 Umwagiliaji	16
4.2 Matumizi ya Pembejeo	17
4.2.1 Kaya zinazotumia Mbegu	17
4.2.2 Eneo Lililopandwa na Kuwekwa Mbolea	18
4.2.3 Eneo lililowekwa Viuatilifu	19
5.0 Upatikanaji wa Huduma za Kifedha (Mikopo)	21
5.1 Upatikanaji wa Mikopo	21
6.0 Hitimisho na Mapendekezo	23

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 2.1:	Idadi na Asilimia ya Kaya za Kilimo kwa Shughuli za Kilimo katika Kipindi cha Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania	2
Jedwali Na. 3.1:	Uzalishaji na Wastani wa Tija wa Mazao ya Nafaka Yaliyochaguliwa Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania	5
Jedwali Na. 3.2:	Uzalishaji na Tija ya Mazao Jamii ya Mizizi Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania	6
Jedwali Na. 3.3:	Uzalishaji na Wastani wa Tija wa Mbegu za Mafuta Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania	6
Jedwali Na. 3.4:	Uzalishaji na Tija ya Mazao Jamii ya Mikunde Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania	7
Jedwali Na. 3.5:	Uzalishaji kwa Baadhi ya Mazao ya Biashara, Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23	8
Jedwali Na. 3.6:	Uzalishaji wa Mazao ya Ndizi, Parachichi na Nyanya katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania	9
Jedwali Na. 4.1:	Eneo lililopandwa, Eneo lililomwagiliwa na Asilimia ya eneo lililopandwa ambalo lilimwagiliwa katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania	16
Jedwali Na. 4.2:	Eneo lilipandwa na Kuwekwa Mbolea katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania	18
Jedwali Na. 4.3:	Eneo na Asilimia ya Eneo Lililowekwa Viutilifu Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania	19

Kielelezo Na. 2.1:	Sehemu ya Hali ya Umiliki wa Ardhi kwa Kaya za Kilimo Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania	3
Kielelezo Na. 2.2:	Sehemu ya Hali ya Umiliki wa Ardhi kwa Mashamba Makubwa Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania	3
Kielelezi Na. 3.1:	Asilimia ya Eneo Lililopandwa Lilioathirika na Majanga Wakati wa Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania	10
Kielelezo Na. 3.2:	Asilimia ya Matumizi ya Mavuno ya Mazao ya Nafaka Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania	11
Kielelezo Na. 3.3:	Asilimia wa Matumizi ya Mavuno ya Mazao Jamii ya Mizizi na Viazi Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania	12
Kielelezo Na. 3.4:	Asilimia ya Matumizi ya Mavuno ya Mazao ya Jamii ya Kunde Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania	12
Kielelezo Na. 3.5:	Asilimia ya Matumizi ya Mavuno ya Mazao ya Mbegu za Mafuta na Karanga Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania	13
Kielelezo Na. 3.6:	Asilimia ya Matumizi ya Mavuno ya Mazao ya Biashara Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania	14
Kielelezo Na. 3.7:	Asilimia ya Matumizi ya Mavuno ya Mazao ya Matunda na Mbogamboga katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania	14
Kielelezo Na. 4.3:	Mtawanyiko kwa Asilimia wa Kaya Zilizotumia Mbegu kwa Aina Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania	17
Kielelezo Na. 5.1:	Asilimia ya Kaya za Kilimo Zenye na Zisizo na Mikopo ya Kilimo kwa Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania	21
Kielelezo Na. 5.2:	Asilimia ya Kaya za Kilimo Zenye Mikopo ya Kilimo kwa Aina ya Mkopesaji kwa Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania	21

Vifupisho vya Maneno

AASS	Utafiti wa Kilimo wa Mwaka
ASLMs	Wizara Zinazoongoza Sekta ya Kilimo
CAADP	Mpango wa Kina wa Maendeleo ya Kilimo Afrika
FAO	Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa
GDP	Pato la Taifa
GSARS	Mkakati wa Kimataifa wa Takwimu za Kilimo na Vijijini
IDA	Shirika la Kimataifa la Maendeleo
NBS	Ofisi ya Taifa ya Takwimu
OCGS	Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar
PO-RALG	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
SDGs	Malengo ya Maendeleo Endelevu
TOE	Mafunzo ya Wadadisi
TOT	Mafunzo ya Wakufunzi
TSMP II	Mpango wa Pili wa Takwimu Tanzania

Dibaji

Kwa furaha kubwa, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) Zanzibar zinawasilisha ripoti ya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka (AASS) kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23. Ripoti hii inatoa takwimu muhimu za kilimo kutoka kwa wakulima wadogo katika ngazi ya kaya na mashamba makubwa kwa lengo la kuarifu sera za serikali, mipango, na programu katika ngazi ya kitaifa na kimkoa. Aidha, ripoti hii inatoa njia ya kutumia takwimu zinazojibu viashiria maalum vya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Mpango wa Kina wa Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP), Dira ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22–2025/26 (FYDP III), Mpango Mkuu wa Taifa wa Takwimu Awamu ya Pili 2022/23–2026/27 (TSMP II), na Mpango Mkakati wa Takwimu za Sekta ya Kilimo 2022/23–2026/27 (ASSP). Juhudi hizi zinalenga kuleta maendeleo endelevu na ustawi katika sekta ya kilimo.

NBS na OCGS zinatoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujitolea na kuunga mkono utafiti wa AASS sambamba na Mpango wa 50 kwa 2030, unaolenga kuziba pengo la takwimu za kilimo kwa kuwezesha nchi 50 zenye kipato cha chini na cha kati kuunda mifumo imara ya kitaifa ya takwimu zinazozalisha na kutumia takwimu za kilimo zenye ubora wa juu na zinazotolewa kwa wakati.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa shukrani za dhati kwa washirika wake hususan Benki ya Dunia, FAO, na IFAD kwa msaada wao wa kifedha na kiufundi ambao umekuwa muhimu katika kuboresha ubora na utoaji wa takwimu za kilimo kwa wakati. Mafanikio ya utafiti wa AASS wa mwaka 2022/23 yanatokana na juhudi za pamoja za wadau mbalimbali, zikiwemo NBS, OCGS na Wizara zinazoongoza Sekta ya Kilimo (ASLMs). Utaalamu wao ulikuwa muhimu katika kuzalisha ripoti ya AASS ya mwaka 2022/23, ambayo ni mzunguko wa kwanza chini ya mpango wa kilimo wa 50x2030.

Mwisho, tunatoa shukrani za dhati kwa wadau wote walioshiriki katika kila hatua ya mchakato wa utafiti, kuanzia maandalizi hadi ripoti ya mwisho. Shukrani maalum ziwaendee wahojiwa wa utafiti, wadadisi, na viongozi wa mitaa na vijiji ambao walijitolea muda na juhudi zao kwa ukarimu, na kufanya ukusanyaji wa takwimu kuwa na mafanikio katika jamii zao. Pamoja, tutaendelea kuzalisha na kuendeleza takwimu za kilimo ili kusaidia maendeleo ya kitaifa na ustawi kwa Watanzania wote.



Dr. Albina Chuwa
Mtakwimu Mkuu wa Serikali
Ofisi ya Taifa ya Takwimu



Salum Kassim Ali
Mtakwimu Mkuu wa Serikali
Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali
Zanzibar

Kumbuka: Matokeo yaliyopatikana kutoka kwenye Utafiti huu hayawezi kulinganishwa moja kwa moja na yale yanayotokana na Vyanzo vya Kiutawala kutokana na mbinu tofauti zinazotumika. Aidha, takwimu za utafiti zinaweza kutumika kuboresha mbinu zinazotumika kushughulikia vyanzo vya takwimu za kiutawala. Kwa ufafanuzi zaidi, tafadhali usisite kuwasiliana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

1.0 Utangulizi

Sekta ya kilimo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa Tanzania, ajira, na kupunguza umasikini, ikichangia takriban asilimia 26.5 ya Pato la Taifa na asilimia 30 ya mauzo ya nje. Kwa kutambua umuhimu wa takwimu sahihi za kilimo kwa ajili ya sera na mipango, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) kwa kushirikiana na wizara zinazoongoza Sekta ya Kilimo (ASLMs) walifanya utafiti wa kila mwaka wa kilimo (AASS) kwa mwaka wa kilimo wa 2022/23. Utafiti huu ulijumuisha kaya za kilimo, matumizi ya ardhi, na uzalishaji wa mazao, mifugo, na uvuvi.

1.1 Dhumuni la Utafiti

Lengo kuu la Utafiti wa Kilimo wa Mwaka (AASS 2022/23) lilikuwa ni kutoa takwimu sahihi kuhusu ukubwa wa ardhi na uzalishaji wa mazao makuu, idadi na bidhaa zitokanazo na mifugo na uvuvi. Takwimu zinazotokana na utafiti huu zinatoa mwanga muhimu kwa wakulima, biashara za kilimo, watunga sera, na wadau wengine muhimu ili kusaidia maamuzi sahihi katika muda mfupi na mrefu.

Malengo mahususi ya AASS 2022/23:

- i. Kukusanya taarifa kwa wakati muafaka kuhusu uzalishaji na tija ya kilimo kwa ngazi ya kitaifa na kimkoa;
- ii. Kutoa takwimu muhimu kwa ajili ya kuendeleza na kuboresha sera za kilimo na kuongoza utekelezaji wa mipango ya kilimo katika ngazi ya kitaifa na kimkoa kati ya sensa moja ya kilimo na nyingine;
- iii. Kuandaa takwimu muhimu zinazoweza kulinganisha maendeleo ya sekta ya kilimo katika maeneo mbalimbali ya nchi.

2.0 Matokeo Muhimu

2.1 Shughuli za Kilimo za Kaya

Matokeo ya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2022/23 (AASS) yanaonesha kuwa, jumla ya kaya 8,970,096 zilijishughulisha na kilimo nchini Tanzania, kati ya hizo kaya 8,814,646 zilikuwa Tanzania Bara na kaya 155,450 zilikuwa Zanzibar. Kati ya jumla ya kaya za kilimo nchini Tanzania, asilimia 98.3 ya kaya zilijihusisha na uzalishaji wa mazao, wakati asilimia 60.6 ya kaya zilijihusisha na ufugaji. Tanzania Bara, asilimia 98.3 ya kaya zilijihusisha na uzalishaji wa mazao wakati asilimia 60.5 ya kaya zilijihusisha na ufugaji. Vivyo hivyo, upande wa Zanzibar, asilimia 97.9 ya kaya zilijihusisha na uzalishaji wa mazao, wakati asilimia 63.4 ya kaya zilijihusisha na ufugaji (Jedwali Na. 2.1).

Jedwali Na. 2.1: Idadi na Asilimia ya Kaya za Kilimo kwa Shughuli za Kilimo katika Kipindi cha Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania


Eneo	Jumla ya Kaya Binafsi ¹	Jumla ya Kaya za Kilimo		Kaya Zilizojishughulisha na Uzalishaji wa Mazao		Kaya Zilizojishughulisha na Ufugaji Mifugo	
		Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia
Tanzania Bara	13,776,975	8,814,646	64.0	8,663,996	98.3	5,335,658	60.5
Zanzibar	375,828	155,450	41.4	152,126	97.9	98,550	63.4
Tanzania	14,152,803	8,970,096	63.4	8,816,122	98.3	5,434,209	60.6

2.2 Umiliki wa Ardhi

Kipindi cha mwaka wa kilimo wa 2022/23, haki ya umiliki wa ardhi kwa njia ya kimila ilikuwa ni Kaya/Shamba Kubwa wa ardhi iliyoongoza kutumika zaidi miongoni mwa kaya za kilimo, ikiwa ni sawa na asilimia 52.3 ya ardhi yote inayomilikiwa nchini Tanzania. Ardhi iliyonunuliwa ilikuwa ni njia ya pili kufuatia katika umiliki wa ardhi ikiwa na asilimia 25.9, wakati ardhi ya makubaliano ya kugawana mavuno ilikuwa na asilimia ndogo zaidi kwa asilimia 0.2 ya ardhi yote inayomilikiwa (Kielelezo Na. 2.1).


¹ Chanzo Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

Kielelezo Na. 2.1: Sehemu ya Hali ya Umiliki wa Ardhi kwa Kaya za Kilimo Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania



Kwa upande wa mashamba makubwa, Haki ya kumiliki ardhi kisheria ilikuwa ndio njia kuu zaidi nchini Tanzania (asilimia 68.4). Aina inayoongoza ya haki za umiliki wa ardhi katika Tanzania Bara ni ule umiliki ardhi wa kisheria (asilimia 68.6), wakati kukodishwa ardhi kutoka kwa wengine ilionekana zaidi upande wa Zanzibar (asilimia 40.0) (Kielelezo Na. 2.2).

Kielelezo Na. 2.2: Sehemu ya Hali ya Umiliki wa Ardhi kwa Mashamba Makubwa Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania



Ujumbe Muhimu:

- *Umiliki wa ardhi kwa njia ya kimila ndiyo aina inayotumika zaidi na kaya za kilimo nchini Tanzania.*
- *Kwa mashamba makubwa, umiliki ardhi kisheria ni aina inayoongoza kutumika zaidi kwa Tanzania Bara, wakati kwa Zanzibar ilikuwa ni kwa kukodishwaa/kutoa ardhi kwa wengine.*

Mtazamo wa Kisera:

Kurasimisha haki za ardhi za kimila ili kuimarisha usalama kwa kaya za kilimo na matumizi endelevu ya ardhi ni muhimu. Haki hizi zilizo na mifumo rasmi ya umiliki wa ardhi zinakuza umiliki salama wa ardhi na kuhimiza uwekezaji na maendeleo ya kilimo.

3.0 Uzalishaji wa Mazao

3.1 Uzalishaji wa Nafaka

Mazao makuu ya nafaka yaliyozalishwa nchini Tanzania katika mwaka wa kilimo wa 2022/23 yalikuwa mahindi, mpunga na mtama. Kwa upande wa Tanzania Bara, mahindi ndiyo yaliyokuwa na uzalishaji mkubwa zaidi (tani 6,970,859), huku mpunga (tani 9,485) ukiongoza kwa uzalishaji ndani ya Zanzibar. Aidha, kwa Tanzania Bara, mpunga ulikuwa na wastani wa juu wa tija (tani 2.2 kwa hekta), wakati Zanzibar, wastani wa juu wa tija mavuno uliripotiwa kwenye mahindi (tani 1.0 kwa hekta) (Jedwali Na. 3.1).

Jedwali Na. 3.1: Uzalishaji na Wastani wa Tija wa Mazao ya Nafaka Yaliyochaguliwa Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania

Kaya/Shamba Kubwa	Zao	Tanzania		Tanzania Bara		Zanzibar	
		Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)	Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)	Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)
Kaya za Kilimo	Mahindi	6,937,553	1.8	6,936,109	1.8	1,444	1.0
	Mpunga	2,413,234	2.2	2,403,783	2.2	9,451	0.8
	Mtama	291,319	1.0	291,146	0.9	173	0.9
	Jumla	9,642,106		9,631,038		11,068	
Mashamba Makubwa	Mahindi	34,753	2.3	34,750	2.3	3	0.5
	Mpunga	30,913	2.7	30,878	2.7	34	0.4
	Mtama	838	0.9	837	0.9	-	-
	Jumla	66,504		66,465		4	
Jumla Kuu	Mahindi	6,972,306	1.8	6,970,859	1.8	1,447	1.0
	Mpunga	2,444,147	2.2	2,434,662	2.2	9,486	0.8
	Mtama	292,157	1.0	291,983	1.0	174	0.9
	Jumla	9,708,610		9,697,504		11,107	

“- “Imeziwa ili kuepuka kufichua takwimu za umiliki wa mtu binafsi au takwimu isiyotosha inayopatikana kutoka kwenye utafiti (Jumla inajumuisha takwimu iliyozuliwa)

3.2 Uzalishaji wa Mazao Jamii ya Mizizi

Mazao ya mizizi yanayolimwa na kaya za kilimo na mashamba makubwa Tanzania ni mihogo, viazi vitamu, na viazi ulaya. Muhogo ulirekodi uzalishaji mkubwa zaidi Tanzania Bara na Zanzibar ukiwa na tani 632,002 na 66,988 mtawaliwa. Licha ya uzalishaji mkubwa, mavuno ya wastani kwa muhogo yalikuwa chini (tani 2.3 /ha) ikilinganishwa na viazi vitamu (tani 2.8 /ha) na viazi mviringo (tani 4.9 /ha) (Jedwali Na. 3.2).

Jedwali Na. 3.2: Uzalishaji na Tija ya Mazao Jamii ya Mizizi Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania

Kaya/Shamba Kubwa	Zao	Tanzania		Tanzania Bara		Zanzibar	
		Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)	Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)	Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)
Kaya	Muhogo	696,447	2.3	631,763	2.3	66,985	2.7
	Viazi vitamu	423,221	2.8	407,442	2.8	15,778	3.4
	Viazi mviringo	529,295	4.9	529,295	4.9	-	-
	Jumla	1,648,963		1,568,500		82,763	
Mashamba Makubwa	Muhogo	242	1.6	239	1.6	3	0.8
	Viazi vitamu	521	3.2	346	3.4	176	2.9
	Viazi mviringo	961	10.5	961	10.5	-	-
Jumla	1,724		1,546		179		
Jumla Kuu	Muhogo	696,689	2.3	632,002	2.3	66,988	2.7
	Viazi vitamu	423,742	2.8	407,788	2.8	15,954	3.4
	Viazi mviringo	530,257	4.9	530,257	4.9	-	-
	Jumla	1,650,688		1,570,047		82,942	

“-” Imezuiwa ili kuepuka kufichua takwimu za umiliki wa mtu binafsi au takwimu isiyotosha inayopatikana kutoka kwenye utafiti (Jumla inajumuisha takwimu iliyozuilwa)

3.3 Uzalishaji wa Mbegu za Mafuta

Katika mwaka wa kilimo 2022/23, alizeti, karanga, na ufuta zilikuwa mbegu kuu za mafuta zilizozalishwa nchini Tanzania. Alizeti ilikuwa na uzalishaji mkubwa zaidi (tani 480,394) na wastani wa tija tani 0.8 kwa hekta, wakati uzalishaji wa karanga ulikuwa tani 412,095 na wastani wa tija wa tani 1.1 kwa hekta. Uzalishaji wa ufuta ulikuwa tani 158,688, na wastani wa tija wa tani 0.6 kwa hekta (Jedwali Na. 3.3).

Jedwali Na. 3.3: Uzalishaji na Wastani wa Tija wa Mbegu za Mafuta Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania

Kaya/Shamba Kubwa	Zao	Tanzania		Tanzania Bara		Zanzibar	
		Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)	Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)	Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)
Kaya	Alizeti	478,080	0.8	478,080	0.8	*	*
	Karanga	411,927	1.1	410,943	1.1	984	1.4
	Ufuta	158,597	0.6	158,597	0.6	*	*
	Jumla	1,048,604		1,047,620		984	
Mashamba Makubwa	Alizeti	2,314	0.7	2,314	0.7	*	*
	Karanga	168	0.6	168	0.6	*	*
	Ufuta	90	0.4	90	0.4	*	*
	Jumla	2,572		2,572		*	
Jumla Kuu	Alizeti	480,394	0.8	480,394	0.8	*	*
	Karanga	412,095	1.1	411,111	1.1	984	1.4
	Ufuta	158,688	0.6	158,688	0.6	*	*
	Jumla	1,051,177		1,050,193		984	

“**” Taarifa haikupatikana kwa Mwaka wa Kilimo 2022/23.

Ujumbe Muhimu

Uzalishaji wa mazao ya nafaka yaliyochaguliwa ni wa juu kwa wakulima wadogo ikilinganishwa na mashamba makubwa.

Mtazamo wa Kisera:

- Serikali iwape wakulima fursa ya kupata huduma za ugani na programu za mafunzo ili kusaidia kusambaza maarifa kuhusu mbinu bora za kilimo, teknolojia mpya na taarifa za masoko.
- Ili kuongeza uzalishaji na tija kwa kiasi kikubwa, serikali iwahamashe wakulima kutumia mbinu za kisasa za kilimo kama vile matumizi ya mbegu zinazozalisha mazao mengi, umwagiliaji sahihi, uwekaji mbolea kwa wakati na udhibiti wa wadudu. Pia serikali inapaswa kuhimiza matumizi ya mashine na vifaa vya kisasa vya kilimo kwa wakulima wadogo na mashamba makubwa ili kusaidia kuongeza ufanisi, kupunguza gharama za uendeshaji, na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao.

3.4 Mazao Jamii ya Mikunde

Mazao ya jamii ya mikunde yaliyozalishwa Tanzania katika kipindi cha mwaka wa kilimo 2022/23 ni maharage, kunde na mbaazi. Maharage yalikuwa na uzalishaji wa tani 678,236 na wastani wa mavuno ya tani 1.2 kwa hekta, mbaazi 144,897 na wastani wa mavuno ya tani 0.4 kwa hekta, na kunde zilikuwa na tani 25,101, na wastani wa mavuno ya tani 0.4 kwa hekta (Jedwali Na. 3.4).

Jedwali Na. 3.4: Uzalishaji na Tija ya Mazao Jamii ya Mikunde Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania

Kaya/Shamba Kubwa	Tanzania			Tanzania Bara		Zanzibar	
	Zao	Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)	Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)	Uzalishaji (tani)	Tija (tani/hekta)
Kaya	Maharage	676,133	1.1	676,128	1.1	*	*
	Kunde	25,088	0.4	24,379	0.4	709	0.5
	Mbaazi	144,790	0.4	144,250	0.4	539	0.5
	Jumla	846,011		844,757		1,248	0
Mashamba Makubwa	Maharage	2,103	-	2,103	1.0	*	*
	Kunde	13	0.8	12	0.8	*	*
	Mbaazi	108	0.6	108	0.6	*	*
	Jumla	2,224		2,223			
Jumla Kuu	Maharage	678,236	1.2	678,236	1.1	*	*
	Kunde	25,101	0.4	24,392	0.4	709	0.5
	Mbaazi	144,897	0.4		0.4	539	0.5
	Jumla	848,234		702,628		1,248	

“*” Takwimu hazipatikani kwa mwaka wa kilimo 2022/23

“-” Imezuiwa ili kuepuka kufichua takwimu za umiliki wa mtu binafsi au takwimu isiyotosha inayopatikana kutoka kwenye utafiti (Jumla inajumuisha takwimu iliyozuilwa).

3.5 Uzalishaji wa Mazao ya Biashara

Katika mwaka wa kilimo wa 2022/23 mazao makuu ya biashara yaliyozalishwa ni pamba, korosho na karafuu. Jumla ya uzalishaji wa pamba ulikuwa tani 218,413 ambapo tani 217,903 zilizalishwa na kaya za kilimo na tani 510 kwa mashamba makubwa. Jumla ya uzalishaji wa korosho ulikuwa tani 135,595, ambapo tani 135,235 zilizalishwa na kaya za kilimo na tani 360 kwa mashamba makubwa. Jumla ya tani 1,840 za karafuu zilizalishwa na kaya za kilimo na mashamba makubwa (Jedwali Na. 3.5).

Jedwali Na. 3.5: Uzalishaji kwa Baadhi ya Mazao ya Biashara, Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23

Mazao	Kaya/Shamba Kubwa	Uzalishaji (tani)
Pamba	Kaya za Kilimo	217,903
	Mashamba Makubwa	510
	Jumla	218,413
Korosho	Kaya za Kilimo	135,235
	Mashamba Makubwa	360
	Jumla	135,595
Karafuu	Kaya za Kilimo	-
	Mashamba Makubwa	-
	Jumla	1,840

*- "Imezuiwa ili kuepuka kufichua takwimu za umiliki wa mtu binafsi au takwimu isiyotosha inayopatikana kutoka kwenye utafiti (Jumla inajumuisha takwimu iliyozuiliwa)

Ujumbe muhimu

Korosho, pamba na karafuu ikiwa ni miongoni mwa mazao makuu ya biashara nchini, kaya za kilimo zimebakia kuwa na mchango mkubwa katika uzalishaji wa mazao hayo ikilinganishwa na mashamba makubwa ambapo mchango wake katika uzalishaji bado ni mdogo.

Mtazamo wa kisera

Mabadiliko ya uzalishaji wa kaya za kilimo kuwa na kilimo cha kisasa na cha kibiashara ni muhimu kuboresha kilimo.

3.6. Uzalishaji wa Migomba, Parachichi na Nyanya

Jumla ya tani 1,352,695 za ndizi zilizalishwa katika Mwaka wa Kilimo 2022/23 nchini Tanzania, ambapo kati ya kiasi hicho kilichozalishwa tani 1,352,281 zilizalishwa na kaya na tani 414 zilizalishwa kutoka mashamba makubwa. Kwa upande wa zao la parachichi, jumla ya tani 75,552 zilizalishwa ambapo kati ya tani zilizozalishwa, tani 67,286 zilizalishwa na kaya na tani 8,266 zilizalishwa kutoka mashamba makubwa. Aidha, kwa zao la nyanya, jumla ya tani 378,778 za nyanya zilizalishwa, ambapo kati ya tani hizo zilizozalishwa, kaya zilizalisha tani 378,318 na mashamba makubwa yalizalisha tani 460 (Jedwali Na. 3.6).

Jedwali Na. 3.6: Uzalishaji wa Mazao ya Ndizi, Parachichi na Nyanya katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania

Kaya za Kilimo/ Mashamba Makubwa	Eneo	Aina ya Zao			Tija (tani/ hekta)
		Ndizi Uzalishaji (tani)	Parachichi Uzalishaji (tani)	Nyanya Uzalishaji (tani)	
Kaya za Wakulima	Tanzania Bara	1,294,765	66,568	343,820	11.5
	Zanzibar	57,516	718	34,498	12.3
	Tanzania	1,352,281	67,286	378,318	11.5
Mashamba Makubwa	Tanzania Bara	413	8,266	438	8.2
	Zanzibar	-	*	22	12.3
	Tanzania	-	8,266	460	8.3
Jumla Kuu	Tanzania Bara	1,295,178	74,834	344,258	11.5
	Zanzibar	57,517	718	34,520	12.3
	Tanzania	1,352,695	75,552	378,778	11.5

“*” Taarifa haikutatikana kwa Mwaka wa Kilimo 2022/23.

“-” Imezuiwa ili kuepuka kufichua takwimu za umiliki wa mtu binafsi au takwimu isiyotosha inayopatikana kutoka kwenye utafiti (Jumla inajumuisha takwimu iliyozuiliwa)

Ujumbe Muhimu:

Kaya za kilimo zimezalisha zaidi ya asilimia 85 ya kiasi chote cha uzalishaji wa ndizi, parachichi na nyanya vilivyozalishwa.


Mtazamo wa Kisera:

Jitihada za Serikali za kuhakikisha teknolojia mbalimbali zinazotokana na matokeo ya tafiti zinawafikia wakulima zidumishwe ili kuongeza tija na uzalishaji kwenye mazao ya matunda na mbogamboga kwa lengo la kutosheleza mahitaji/masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

3.6 Majanga kwenye Eneo Lililopandwa Mazao

Katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, katika msimu wa mvua za vuli, asilimia 9.5 ya eneo lote lililopandwa na kaya za kilimo liliathiriwa kikamilifu na majanga, na asilimia 25.8 iliathiriwa kwa kiasi. Kwa mashamba makubwa, asilimia 21.6 yaliathirika kikamilifu, huku asilimia 9.2 yaliathirika kwa kiasi. Katika mvua za masika, asilimia 11.0 ya eneo lililopandwa na kaya za kilimo liliathiriwa kikamilifu na asilimia 31.4 iliathirika kwa kiasi. Katika msimu huo huo, asilimia 9.7 ya eneo lote lililopandwa na mashamba makubwa liliathiriwa kikamilifu, huku asilimia 13.2 iliathirika kwa kiasi (Kielelezo Na. 3.1).

Kielelezi Na. 3.1: Asilimia ya Eneo Lililopandwa Lilioathirika na Majanga Wakati wa Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania



Ujumbe Muhimu:

Katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, majanga yaliathiri kwa kiasi kikubwa kaya za kilimo na mashamba makubwa nchini Tanzania, huku sehemu kubwa ya eneo lililopandwa na mashamba makubwa likiathirika kikamilifu katika msimu wa mvua za vuli.

Mtazamo wa Kisera:


- Kuimarisha Mifumo ya Tahadhari ya Mapema kwa ajili ya utoaji wa taarifa za tahadhari kwa wakati juu ya mabadiliko ya tabia nchi na hali ya hewa.*
- Mbinu mbadala za usimamizi wa majanga na kupunguza athari zake katika kilimo zinapaswa kuboreshwa.*

3.7 Matumizi ya Mazao

3.7.1 Nafaka

Matokeo yanaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 80.0 ya mazao ya nafaka yaliozalishwa na kaya za kilimo yalitumiwa na kaya au kuuzwa bila kusindika. Kwa mashamba makubwa, kiasi cha mavuno yaliyouzwa bila kusindikwa kilianza asilimia 49.0 hadi asilimia 75.0 (Kielelezo Na. 3.2).


Kielelezo Na. 3.2: Asilimia ya Matumizi ya Mavuno ya Mazao ya Nafaka Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania



3.7.2 Mazao Jamii ya Mizizi na Viazi

Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 72.7 ya viazi vitamu na asilimia 62.9 ya mihogo iliyozalishwa na kaya za kilimo ilitumika kwa matumizi ya kaya. Hata hivyo, sehemu kubwa ya viazi mviringo/mbatata (asilimia 78.1) viliuzwa bila kusindikwa. Kwa mashamba makubwa, viazi mviringo/mbatata vingi vilivyovunwa (asilimia 96.9) viliuzwa bila kusindikwa, wakati mihogo na viazi vitamu kila moja ilikuwa na asilimia 50.7 ya mavuno yake na yalielekezwa kwenye matumizi mengine (Kielelezo Na. 3.3).


Kielelezo Na. 3.3: Asilimia wa Matumizi ya Mavuno ya Mazao Jamii ya Mizizi na Viazi Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania



3.7.3 Mazao Jamii ya Kunde

Matokeo ya utafiti wa Kilimo 2022/23 yanaonesha kuwa, Matumizi makubwa ya mazao ya jamii ya kunde yaliovunwa na kaya za kilimo yalitumika kwa matumizi ya kaya au kuuzwa bila kusindika. Kunde ndizo zilizoongoza kutumiwa na kaya kwa (asilimia 61.9), wakati mbaazi ziliuzwa bila kusindikwa kwa (asilimia 71.4). Wakati, kwa mashamba makubwa, zaidi ya asilimia 85.0 ya mazao ya kunde yaliuzwa bila kusindikwa, wakati sehemu iliyobaki ilitumika kwa matumizi mengine (Kielelezo Na. 3.4).


Kielelezo Na. 3.4: Asilimia ya Matumizi ya Mavuno ya Mazao ya Jamii ya Kunde Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania



3.7.4 Mbegu za Mafuta na Karanga

Karanga, ufuta na alizeti ndiyo mazao makuu ya mbegu za mafuta na karanga yaliyoripotiwa katika mwaka wa kilimo wa 2022/23. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa zaidi ya asilimia 50.0 ya mbegu za mafuta na karanga zilizovunwa na kaya za kilimo na mashamba makubwa ziliuzwa bila kusindikwa (Kielelezo Na. 3.5).


Kielelezo Na. 3.5: Asilimia ya Matumizi ya Mavuno ya Mazao ya Mbegu za Mafuta na Karanga Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania



3.7.5 Mazao ya Biashara

Katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, karafuu, pamba, na korosho ni miongoni mwa mazao makuu ya biashara yaliyozalishwa na Kaya za kilimo na mashamba makubwa. Matokeo yanaonesha kuwa zaidi ya asilimia 80 ya mazao yaliyovunwa na kaya za kilimo na mashamba makubwa yaliuzwa bila kusindikwa (Kielelezo Na. 3.6).


Kielelezo Na. 3.6: Asilimia ya Matumizi ya Mavuno ya Mazao ya Biashara Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania



3.7.6 Matunda na Mbogamboga

Katika mwaka wa kilimo wa 2022/23, zaidi ya asilimia 50 ya parachichi na nyanya ziliuzwa bila kusindikwa huku asilimia 54.7 ya ndizi zililiwa na kaya na asilimia 42.4 ziliuzwa bila kusindikwa. Kwa mashamba makubwa, parachichi, ndizi na nyanya, kila moja lilikuwa na zaidi ya asilimia 75 ya mavuno yaliyotumika yakiwa hayajasindikwa (Kielelezo Na. 3.7).

Kielelezo Na. 3.7: Asilimia ya Matumizi ya Mavuno ya Mazao ya Matunda na Mbogamboga katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania



Ujumbe Muhimu:

Sehemu kubwa zaidi ya mavuno ya mazao hutumika kwa matumizi ya kaya au kuuzwa bila kusindika. Hii inabaki kuwa muhimu kwa kaya zote za kilimo na mashamba makubwa.

Mapendekezo ya Kisera:

- *Kuhimiza matumizi jumuishi/mseto katika bidhaa za kilimo zisizo asilia ili kuongeza thamani na ubora wa mazao ya kilimo.*
- *Kuimarisha usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuongeza thamani wa mazao ya kilimo na mapato ya shambani.*

4.0 Umwagiliaji na Matumizi ya Pembejeo

4.1 Umwagiliaji

Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 3.5 ya eneo lote lililopandwa mazao katika mwaka wa kilimo 2022/23 lilimwagiliwa. Katika eneo lote lililopandwa mazao na kaya za kilimo, asilimia 3.0 lilimwagiliwa, wakati eneo lililomwagiliwa kwa upande wa mashamba makubwa ilikuwa asilimia 28.2 ya eneo lililopandwa (Jedwali Na. 4.1).

Jedwali Na. 4.1: Eneo lililopandwa, Eneo lililomwagiliwa na Asilimia ya eneo lililopandwa ambalo lilimwagiliwa katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania

Kaya za Kilimo/ Mashamba Makubwa	Eneo	Eneo lililopandwa (hekta)	Eneo lilomwagiliwa	
			Eneo (hekta)	Asilimia
Kaya za Kilimo	Tanzania Bara	16,726,471	482,257	2.9
	Zanzibar	134,997	15,870	11.8
	Tanzania	16,861,468	498,127	3.0
Mashamba Makubwa	Tanzania Bara	376,125	107,033	28.5
	Zanzibar	3,149	35	1.1
	Tanzania	379,274	107,068	28.2
Wamiliki wote	Tanzania Bara	17,102,596	589,290	3.4
	Zanzibar	138,146	15,905	11.5
	Tanzania	17,240,742	605,195	3.5

Ujumbe Muhimu:

Asilimia ya eneo la umwagiliaji kati ya eneo lililopandwa mazao na kaya za kilimo bado ni ndogo ikilinganishwa na mashamba makubwa.

Mtazamo wa Kisera:


- Ushiriki wa Sekta ya Umma na Binafsi katika maendeleo ya tasnia ya umwagiliaji nchini unapaswa kukuzwa ili kuhakikisha panakuwepo na uwezo wa kutosha na wa kiutaalam katika maendeleo na usimamizi endelevu wa skimu za umwagiliaji.*
- Maendeleo ya mbinu za uvunaji maji kwa njia ya kiuchumi, inayokubalika kijamii na inayozingatia mazingira inapaswa kuendelea kuimarishwa katika kaya za kilimo.*

4.2 Matumizi ya Pembejeo

4.2.1 Kaya zinazotumia Mbegu

Matokeo yanaonesha kuwa, asilimia 41.3 ya kaya zinazolima mazao Tanzania zilitumia mbegu zilizoboreshwa. Hata hivyo, matumizi ya mbegu za asili yamekuwa ya juu zaidi nchini (asilimia 79.6) ikilinganishwa na mbegu zilizoboreshwa, hilo limeonekana pia kwa Tanzania Bara (asilimia 79.9) na Zanzibar (asilimia 66.6). Kuhusu matumizi ya mbegu zilizoboreshwa na zile ziliboreshwa na kurudiwa tena, mbegu zilizoboreshwa zilitumika kwa kiwango kikubwa zaidi Tanzania Bara (asilimia 41.1), na mbegu zilizoboreshwa na kurudiwa tena zikionesha kutumika zaidi (asilimia 38.7) kwa upande wa Zanzibar (Kielelezo Na. 4.3).

Kielelezo Na. 4.3: Mtawanyiko kwa Asilimia wa Kaya Zilizotumia Mbegu kwa Aina Katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania



Ujumbe Muhimu:

Matokeo yanonesha kuwa, matumizi ya mbegu zilizoboreshwa bado yapo chini ikilinganishwa na ya mbegu za asili.

Mtazamo wa Kiseri:

- *Ni muhimu kwa Serikali kuendelea na jitihada za kuhamasisha matumizi ya pembejeo za kisasa ikiwemo mbegu bora.*
- *Uhamasishaji wa uzalishaji, usambazaji na matumizi ya mbegu bora uendelee kufanyika kwa kushirikisha Sekta ya Umma na Binafsi.*

4.2.2 Eneo Lililopandwa na Kuwekwa Mbolea

Matokeo yanaonesha kuwa, asilimia 32.1 ya eneo lililopandwa nchini katika Mwaka wa Kilimo wa 2022/23 liliwekwa mbolea. Aidha, asilimia 31.5 ya eneo lililopandwa na kaya za kilimo liliwekwa mbolea, wakati asilimia 61.4 ya eneo lililopandwa la mashamba makubwa liliwekwa mbolea (Jedwali Na. 4.2).

Jedwali Na. 4.2: Eneo lililopandwa na Kuwekwa Mbolea katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania

Eneo	Kaya za Kilimo/ Mashamba Makubwa	Eneo liliopandwa (ha)	Eneo Lililopandwa na Kuwekwa Mbolea	
			(ha)	Asilimia
Tanzania Bara	Kaya	16,726,471	5,265,761	31.5
	Mashamba Makubwa	376,125	231,128	61.4
	Jumla	17,102,596	5,496,889	32.1

Zanzibar	Kaya	134,997	43,886	32.5
	Mashamba Makubwa	3,149	1,737	55.2
	Jumla	138,146	45,623	33.0
Tanzania	Kaya	16,861,468	5,309,646	31.5
	Mashamba Makubwa	379,274	232,865	61.4
	Jumla	17,240,742	5,542,512	32.1

Ujumbe Muhimu:

Karibia theluthi moja ya eneo lililolimwa na kaya liliwekwa mbolea na theluthi mbili ya eneo la mashamba makubwa liliwekwa mbolea.

Mtazamo wa Kisera:

Inaonekana kuwa jitihada zinazofanywa na Serikali za kutoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima ni muhimu katika kuhakikisha upatikanaji na matumizi ya mbolea kwa kaya.

4.2.3 Eneo lililowekwa Viuatilifu

Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 32.7 ya eneo lote lililopandwa mazao Tanzania liliwekwa viuatilifu. Eneo lililowekwa viuatilifu kwa upande wa mashamba makubwa ilikuwa asilimia 65.5 ya eneo lililopandwa, wakati kwa upande wa kaya za kilimo ilikuwa asilimia 31.9 (Jedwali Na. 4.3).

Jedwali Na. 4.3: Eneo na Asilimia ya Eneo Lililowekwa Viuatilifu Katika Mwaka wa Kilimo 2022/23, Tanzania

Kaya za Kilimo/ Mashamba Makubwa	Eneo	Eneo lililopandwa (hekta)	Eneo lililowekwa Viuatilifu	
			Eneo (hekta)	Asilimia
Kaya za Kilimo	Mainland Tanzania	16,726,471	5,366,347	32.1
	Zanzibar	134,997	17,511	13
	Tanzania	16,861,468	5,383,858	31.9
Mashamba Makubwa	Mainland Tanzania	376,125	246,852	65.6
	Zanzibar	3,149	1,677	53.2

	Tanzania	379,274	248,529	65.5
Wamiliki wote	Mainland Tanzania	17,102,596	5,613,199	32.8
	Zanzibar	138,146	19,188	13.9
	Tanzania	17,240,742	5,632,387	32.7

Ujumbe Muhimu:

- *Sehemu ya eneo lililowekwa viuatilifu ni kubwa katika mashamba makubwa kuliko katika kaya za kilimo.*
- *Sehemu ya eneo lililowekwa viuatilifu ni kubwa zaidi Tanzania Bara kuliko Zanzibar.*

Mtazamo wa Kisera:


- *Juhudi zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine muhimu wanaohusika na huduma za afya ya mimea ni muhimu katika kupambana na wadudu na milipuko ya magonjwa.*
- *Ni muhimu kuimarisha ufuatiliaji, mfumo na njia za kudhibiti wadudu na magonjwa kwa upande wa kaya za kilimo na mashamba makubwa.*

5.0 Upatikanaji wa Huduma za Kifedha (Mikopo)

5.1 Upatikanaji wa Mikopo

Nchini Tanzania, asilimia 4.9 ya kaya za kilimo zilichukua mikopo kwa madhumuni mbalimbali ya kilimo ambapo Tanzania Bara ilikuwa na kiwango cha juu zaidi kwa asilimia 5.0 ya kaya za kilimo zilizopata mkopo, wakati Zanzibar ilikuwa na kiwango cha chini zaidi cha asilimia 0.7 (Kielelezo Na. 5.1).


Kielelezo Na. 5.1: Asilimia ya Kaya za Kilimo Zenye na Zisizo na Mikopo ya Kilimo kwa Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania



5.2 Watoa Mikopo

Watoa mikopo walioonekana kwa wingi kwa kaya za kilimo nchini Tanzania walikuwa wakopeshaji binafsi (asilimia 29.7), marafiki au familia wanaoishi nchini (asilimia 21.1), na taasisi za fedha ndogo ndogo (asilimia 18.7), huku kampuni za bima zikiwa na asilimia 0.2. Usambazaji sawa wa watoa mikopo ulionekana katika Tanzania Bara, wakati Zanzibar, taasisi za fedha ndogo ndogo (asilimia 29.3) na mashirika yasiyo ya kiserikali (asilimia 21.0) zilikuwa na jukumu kubwa zaidi katika kutoa mikopo (Kielelezo Na. 5.2).

Kielelezo Na. 5.2: Asilimia ya Kaya za Kilimo Zenye Mikopo ya Kilimo kwa Aina ya Mkopeshaji kwa Mwaka wa Kilimo wa 2022/23, Tanzania



6.0 Hitimisho na Mapendekezo

Kilimo kina nafasi muhimu katika uchumi wa Tanzania, ambapo asilimia 63.4 ya kaya zinajihusisha na shughuli za kilimo kama uzalishaji wa mazao na ufugaji. Licha ya umuhimu wake, kaya za kilimo zinakabiliwa na changamoto kama vile usalama mdogo wa umiliki wa ardhi, matumizi madogo ya mbinu za kisasa za kilimo, hatari za mabadiliko ya hali ya hewa, na upatikanaji mdogo wa huduma za kifedha. Vigezo hivi vinakwamisha uzalishaji na ukuaji wa uchumi.

Mapendekezo:

- i. **Uwekezaji katika Kilimo:** Kutoa kipaumbele kwa uwekezaji katika kilimo ili kuongeza maendeleo ya kiuchumi. Kuwasaidia wakulima wadogo na wakubwa kwa upande wa rasilimali na miundombinu;
- ii. **Usalama wa Umiliki wa Ardhi:** Kurasimisha haki za ardhi za kimila ili kuhakikisha umiliki na kuhamasisha uwekezaji wa kilimo. Kuhakikisha mifumo ya umiliki wa ardhi ni imara na inasaidia matumizi endelevu ya ardhi;
- iii. **Mbinu za Kisasa za Kilimo:** Wakulima wapewe mafunzo na huduma za ugani. Kuhimiza matumizi ya mbegu bora, umwagiliaji wa kisasa, na mashine za kisasa ili kuongeza uzalishaji;
- iv. **Kilimo Biashara:** Kuhimiza mabadiliko chanya katika kaya za kilimo kuhama kutoka kwenye kilimo cha kujikimu na kuelekea kwenye kilimo cha biashara;
- v. **Utafiti na Ubunifu:** Kuendeleza programu za utafiti ili kuboresha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kukidhi mahitaji ya ndani na nje;
- vi. **Ustahimilivu wa Hali ya Hewa:** Kuimarisha mifumo ya kutoa tahadhari mapema kwa mabadiliko ya hali ya hewa na kukuza mikakati ya usimamizi wa hatari zinazotokana na hali ya hewa ili kupunguza hasara katika kilimo;
- vii. **Onguzo la Thamani:** Kuhimiza utofauti na usindikaji wa mazao ili kuongeza thamani na ubora wa bidhaa za kilimo, na kuongeza kipato cha wakulima;
- viii. **Maendeleo ya Umwagiliaji:** Kuhimiza ushiriki wa sekta ya umma na binafsi katika miradi ya umwagiliaji na utumiaji endelevu wa maji;
- ix. **Matumizi ya Mbegu Bora:** Kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kisasa kama mbegu bora kupitia ushirikiano kati ya sekta za umma na binafsi;
- x. **Upatikanaji wa Fedha/Mikopo:** Kuimarisha taasisi za kifedha na kutoa elimu ya programu za kifedha ili kuhakikisha wakulima wanaweza kupata huduma muhimu za kifedha.

Kwa kutekeleza mapendekezo haya, Tanzania inaweza kuongeza uzalishaji wa kilimo, kuhakikisha usalama wa chakula, na kuchochea ukuaji wa uchumi.

MUHTASARI WA VIASHIRIA MUHIMU KWA MWAKA WA KILIMO 2022/23

Kiashiria	Tanzania	Tanzania Bara	Zanzibar
Kaya za Kilimo Zinazojishughulisha na Shughuli za Kilimo			
Uzalishaji wa Mazao (asilimia)	98.3	98.3	97.9
Ufugaji wa Mifugo (asilimia)	60.6	60.5	63.4
Sehemu ya Umiliki wa Ardhi na Kaya za Kilimo (asilimia)			
Haki za kimila za kumiliki	52.3	52.3	44.3
Haki zilizotolewa za kumiliki	0.9	0.8	5.4
Kununuliwa	25.9	25.9	16.3
Kupangishwa	10.3	10.3	1.5
Kugawana	0.2	0.2	0.3
Kukopeshwa bure	4.9	4.8	28.5
Kuingia bila ruhusa	3.3	3.3	2.4
Haki za ardhi za pamoja	1.0	1.3	2.4
Nyingine	1.0	1.1	0.5
Uzalishaji wa Mazao kwa Ngazi ya Kaya			
<i>Tija ya Mazao Makuu ya Nafaka</i>			
Mahindi (tani/ha)	1.8	1.8	1.0
Mpunga (tani/ha)	2.2	2.2	0.8
Mtama (tani/ha)	1	0.9	0.9
Uwele (tani/ha)	0.8	0.8	1.6
<i>Tija ya Mazao Mzizi na Muhogo</i>			
Muhogo (tani/ha)	2.3	2.3	2.7
Viazi vitamu (tani/ha)	2.8	2.8	3.4
Viazi mviringo (tani/ha)	4.9	4.9	-
Cocoyams (tani/ha)	2.5	2.5	-
<i>Tija ya Mazao ya Mbegu za Mafuta</i>			
Alizeti (tani/ha)	0.8	0.8	*
Karanga (tani/ha)	1.1	1.1	1.4
Ufuta (tani/ha)	0.6	0.6	*
<i>Tija ya Mazao ya Mikunde</i>			
Maharage (tani/ha)	1.1	1.1	*
Cowpeas (tani/ha)	0.4	0.4	0.5
Njugu (tani/ha)	0.4	0.4	0.5
<i>Tija ya Mazao ya Biashara</i>			
Pamba (tani/ha)	0.7	0.7	*
Korosho (tani/ha)			
Karafuu (tani/ha)			
<i>Tija ya Mazao ya Matunda na Mbogamboga</i>			
Ndizi (tani/ha)			
Parachichi (tani/ha)			
Nyanya (tani/ha)	11.5	11.5	12.3

Kiashiria	Tanzania	Tanzania Bara	Zanzibar
Eneo Lililopandwa Lililopata Athari (Mazingira/Zisizo za Mazingira)			
<i>Msimu wa Vuli</i>			
Sehemu yote ya athari (asilimia)	9.5		
Sehemu ya athari (asilimia)	25.8		
<i>Msimu wa MASika</i>			
Sehemu yote ya athari (asilimia)	11		
Sehemu ya athari (asilimia)	31.4		
Umwagiliaji			
Eneo lililopandwa mazao (ha)	16,861,468	16,726,471	134,997
Jumla ya eneo lililomwagiliwa (asilimia)	3.0	2.9	11.8
Matumizi ya Mbegu kwa Kaya			
<i>Matumizi ya Mbegu</i>			
Mbegu bora (asilimia)	41.3	41.6	18.9
Mbegu za asili (asilimia)	79.6	79.9	66.6
Mbegu zilizoboreshwa zilitumika tena (asilimia)	17.5	17.2	38.7
Eneo Lililowekwa Mbolea (ha)	5,542,512	5,496,889	45,622
Eneo Lililowekwa Viutilifu (Pesticides) (ha)	5,383,858	5,366,347	17,511
Upatikanaji wa Mikopo kwa Kaya za Kilimo			
<i>Mikopo iliyoombwa kwa madhumuni ya kilimo (asilimia)</i>	4.9	5.0	0.7
<i>Chanzo cha Mkopo kwa Kaya za Kilimo</i>			
Benki za umma au taasisi za serikali (asilimia)	5.4	5.3	15.6
Benki za biashara (asilimia)	5.1	5	11.8
Kampuni za bima (asilimia)	0.2	0.2	0
Taasisi ndogo za mikopo (asilimia)	18.7	18.7	29.3
Asasi zisizo za kiserikali (NGOs) (asilimia)	7.0	7.0	21
Vyama vya uzalishaji (asilimia)	11.5	11.5	14.5
Wakopesaji binafsi (asilimia)	29.7	29.8	1
Marafiki au familia - wanaoishi nchini (asilimia)	21.1	21.2	6.9
Marafiki au familia - wanaoishi nje ya nchi (asilimia)	0.3	0.3	0
Nyingine (asilimia)	1.0	1.0	0
Sababu za Kutokukopa Fedha (Mkopo)			
Hawakutuma maombi (asilimia)	77.5	77.3	88
Maombi yalikataliwa (asilimia)	0.8	0.8	1.9
Haiwezekani kuomba, hakuna upatikanaji (asilimia)	3.1	3.2	0.3
Shughuli ya uwekezaji haikubaliki (asilimia)	0.7	0.7	0
Kipato hakitoshelezi (asilimia)	7.6	7.6	5.1
Historia mbaya ya mikopo (asilimia)	1.5	1.5	0.1
Dhamana haitoshi (asilimia)	0.8	0.8	0.1
Kiwango cha riba ni kikubwa (asilimia)	2.4	2.4	0.3
Nyingine (asilimia)	5.6	5.7	4.2

“**” Taarifa haikutikana kwa Mwaka wa Kilimo 2022/23.

“- “Imewekwa kando ili kuepuka kufichua data za umiliki binafsi au data haitoshi kutoka kwenye utafiti (Jumla inajumuisha data iliyowekwa kando).”

